



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR  
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

---

**TAARIFA YA SERIKALI KUHUSIANA NA MWENENDO  
WA MRIPUKO WA VIRUSI YVA KORONA  
LEO TAREHE 23 MACHI, 2020**

**Ndugu Wananchi,**

Kama mnavyofahamu, Dunia imekumbwa na maradhi ya ungojwa wa Virusi ya CORONA.

Wakati tunaendelea kuchukua tahadhari kuzuia kusambaa kwa maradhi haya, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaagiza yafuatayo ili kuendelea kujikinga na kukabiliana na mripuko wa maradhi haya.

1. Katika masoko yote watu wanunue na kuondoka haraka baada ya kupata huduma, ni marufuku kufanya soko kuwa ni sehemu ya mazungumzo.
2. Masoko yote yanapaswa kutoa huduma kuanzia asubuhi hadi 12:00 jioni na si vyenginevyo, ambapo katika suala hili mabaraza ya Manispaa na Halmashauri wanatakiwa kusimamia agizo hili mara moja.
3. Kufunga baa na kumbi za starehe hadi hapo itakapotolewa taarifa nyengine.
4. Serikali bado inasisitiza kuzuia mikusanyiko inayokutanisha watu wengi kwa wakati mmoja ikiwemo mkutano, warsha, makongamano, semina sherehe za harusi, za kifamilia, michezo na burudani na Viongozi wote wa Mikoa na Wilaya wanatakiwa wasimamie agizo hili.

**AHSANTENI**

**MOHAMED ABOUD MOHAMED  
WAZIRI WA NCHI  
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS  
ZANZIBAR.**

---

*Kwa mawasiliano ya moja kwa moja:*

*Waziri wa Nchi 024 22 33100; Katibu Mkuu 024 22 30808; Naibu Katibu Mkuu 024 22 30937*